**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 12 Juni, 2023**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

148. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Miongoni mwa mabadiliko yaliyofanywa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kubadilisha Sera yetu ya Mambo ya Nje kuwa ya kuleta tija kiuchumi badala ya kuegemea katika siasa pekee. Katika hatua hii ndipo tulipoanzisha Diplomasia ya Uchumi ambayo sasa ndio Sera yetu ya Kimataifa.

Je, kwa kiasi gani diplomasia mpya ya uchumi inachangia kuleta mapinduzi ya viwanda na kilimo hapa nchini.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

198. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Pamoja na jitihada za Serikali katika kuimarisha matumizi bora ya ardhi nchini, bado kuna changamoto katika matumizi hayo na pia katika kuheshimiwa kwa haki ya ardhi. Katika kutatua changamoto hizo.

(a) Je, kwa mwaka 2022/2023, Serikali imetekeleza vipi mpango wa mazingira na hifadhi ya ardhi kuzuia mmong'onyoko wa ardhi na fukwe.

(b) Je, kwa mwaka 2022/2023, Serikali inasimamia vipi utekelezaji wa mikakati ya kudhibiti na kuvihifadhi visiwa vidogo vidogo.

(c) Je, kwa mwaka 2022/2023, Serikali imeutekeleza vipi Mpango Mkuu (Master Plan) wa Zanzibar nzima na kwa kiasi gani Serikali imeweza kuzuia matumizi mabaya ya ardhi kwa kupitia mpango huo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

127. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Pamoja na maelezo mengi ya kisiasa ambayo Serikali inayatoa mara kwa mara kuhusiana na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) huku kwa upande wa Tanzania bara kukiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), bado wananchi walio wengi hawafahamu kwa ufasaha mtazamo wa kiuchumi juu ya haja ya kuanzishwa ZRA.

(a) Je, ni lini Serikali itaondoa utitiri wa kodi kwa wafanyabiashara na kuweka mfumo bora wa ulipaji kodi wa kituo kimoja (One Tax Centre).

(b) Je, Serikali inaona ubaya gani wa kuwa na chombo kimoja cha ukusanyaji na usimamizi wa kodi na mapato Zanzibar.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba ZRA inaanzisha chuo/vyuo vyake kama ilivyo kwa TRA.

**Wizara ya Afya:**

77. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuna taarifa kuwa Divisheni ya Afya ya Akili ya Hospitali ya Kidongo Chekundu, inakabiliwa na uhaba wa dawa zinazotumiwa kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa walioathirika na uraibu wa dawa za kulevya kwa muda mrefu.

(a) Je, kwa kiasi gani suala hili lina ukweli.

(b) Je, Wizara yako imechukua hatua gani kutatua tatizo hilo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

210. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo la kufurahisha kwamba Serikali ilianzisha utaratibu wa malipo kwa huduma zinazopita bandarini Zanzibar katika kituo kimoja (One Stop Centre). Hata hivyo, bado haijaeleweka uhusiano wa kituo hicho na malipo ya huduma za matumizi ya bandari (wharfage charges) ambazo msafiri hutakiwa kulipa kila upande kati ya Unguja na Pemba kwa safari moja.

(a) Je, kiwango gani cha mzigo wa abiria (ujazo na uzito) anayesafiri kwa meli kati ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam kinaruhusiwa bila ya malipo ya matumizi ya bandari (Wharfage) na meli (Transportation Fee).

(b) Je, kwa nini abiria wanaosafiri na mizigo (ikiwemo mizigo midogo ya binafsi) kati ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam hulazimishwa kulipia malipo ya matumizi ya bandari (Wharfage) pande zote mbili za safari.

(c) Je, kiwango gani cha mzigo kinachopaswa kulipiwa, na kwa nini Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) haliruhusu malipo ya jumla ya matumizi ya bandari (Wharfage) upande mmoja tu wa safari.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

139. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Sera ya Kilimo ni miongoni mwa sera zenye kuonesha dira na mwelekeo mzima wa namna gani Serikali yetu imejipanga katika kuinua kilimo nchini.

Je, Sera ya Kilimo inakidhi vipi mabadiliko ya teknolojia mbali mbali zinazofungamana na kilimo cha kisasa.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

199. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali inajitahidi sana katika kutatua migogoro inayohusu umiliki wa ardhi na pia katika kupatikana makaazi bora ya kisasa na bei nafuu. Hata hivyo, kutotumia teknolojia ya kisasa kwa kiasi kikubwa kumerejesha nyuma juhudi za Serikali ikiwemo uzalishwaji wa migogoro zaidi baada ya kutatua mgogoro mmoja.

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani kwa mwaka 2022/2023 wa kutumia teknolojia endelezi na endelevu katika kuhakikisha kuwa kunapatikana makaazi bora ya kisasa na bei nafuu bila ya kuzalisha migogoro mipya ya ardhi.

(b) Je, kwa kiasi gani utekelezaji wa mpango mkakati wa matumizi bora ya ardhi kwa mwaka 2022/2023 umejali maslahi ya wananchi wanyonge.

(c) Je, kwa mwaka 2022/2023, hali ya kupatikana ardhi na hati za umiliki bila ya masharti magumu imefikia kiwango gani.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

145. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali katika suala zima la Uchumi wa Buluu kupitia sekta ya uvuvi, bado suala la uvuvi haramu ni changamoto inayokwaza maendeleo ya sekta hiyo.

Kwa kiasi gani Serikali imeweza kudhibiti suala la uvuvi haramu.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

161. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Utalii wa ndani bado haujapata hamasa na muamko wa kutosha kwa wananchi wetu kutembelea kwa wingi kwenye vivutio na maeneo yetu ya kihistoria licha ya kukua na kuimarika kwa sekta ya utalii hapa nchini mwetu.

(a) Je, ni yepi mafanikio yanayotokana na utalii wa ndani hadi hivi sasa.

(b) Ni sababu zipi zinazopelekea kukosekana kwa hamasa na muamko pamoja na muitiko mzuri kwa wananchi wetu kufanya utalii wa ndani.

(c) Je, Wizara inalihimiza na kulihamasisha vipi swali hili la utalii wa ndani kutokana na umuhimu wake.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**12 Juni, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**